



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI UKAGUZI WA VITUO VINAVYOTOA HUDUMA ZA AFYA

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ipo katika zoezi la kukagua vituo vya afya nchini vinavyotoa huduma za afya zikiwemo hospitali, zahanati na maabara. Zoezi hili linaloendelea nchini lina lengo la kuhakikisha pamoja na mambo mengine taratibu zilizowekwa za utoaji wa huduma bora za afya zinafuatwa na kuzingatiwa na vituo hivyo pia kubaini vituo ambavyo vimekuwa vikitoa huduma kinyume na taratibu za utoaji wa huduma za afya ili wachukuliwe hatua zinazostahili. Hii ni hatua ya nzuri na ya kupongezwa kwani huhakikisha uwepo wa huduma bora za afya kwa wananchi ambazo zinakidhi haja na matakwa ya watanzania.

Kwa muda mrefu huduma za afya nchini zimekuwa zikizembewa na kutolewa chini ya kiwango hali inayosababishwa na kuwepo kwa wafanyakazi wasio na sifa, mazingira yasiyoridhisha ya utoaji huduma, vifaa duni na muda mwingine matumizi ya madawa yaliyokatazwa au yaliyoisha muda wake. Hali hii haijionyeshi katika vituo binafsi pekee bali hata vile vituo vya serikali ambavyo serikali yenyewe inasimamia na kuviendesha. Athari kutokana na hali hii ya kutoa huduma isiyo ridhisha ni kubwa kwani sio tu hudhorotesha huduma za afya nchini bali pia husababisha vifo na hivyo taifa kupoteza nguvu kazi ambayo ingetumika katika kuleta maendeleo nchini.

Hivyo, hatua hii ya kuhakiki uendeshaji wa vituo hivi vya afya hauna budi kupongezwa kwani ni juhudi zenye manufaa kwa taifa letu zinazolenga kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini. Hata hivyo, pamoja na kazi nzuri Serikali inafanya kupitia Wizara ya afya na Ustawi wa Jamii, tunapendekeza serikali kutofanya ukaguzi huo katika vituo vya afya vinavyomilikiwa na watu binafsi au mashirika binafsi tu ila ifanye ukaguzi pia katika upande wa vituo vinavyomilikiwa na Serikali

Tunapendekeza kuwa serikali isilenge tu kuvifungia vituo vinavyobainika kuwa na mapungufu ila kuwepo na upembuzi yakinifu ili kuweza kuviimarisha na kuvijengea uwezo ili kutoa huduma bora za afya yenye tija kwa wananchi wanaozunguka katika eneo husika.

Tunashauri pia, zoezi hili la ukaguzi lifanyike nchi nzima na liwe la kudumu na pia tunashauri uwepo usimamizi madhubuti wa kuhakiki vibali au leseni zinazotolewa kwa ajili ya kuendesha huduma za afya zikiwemo hospitali, zahanati, maabara na maduka ya dawa.

Na mwisho, tunaishauri serikali iwe na mpango madhubuti wa kuimarisha huduma za afya zinazotolewa na serikali katika vituo vyake vya afya ambazo hutumiwa na watu wengi kuliko kuangalia upande mmoja wa sekta binafsi ambao unatumiwa na watu wachache wenye uwezo wa kumudu gharama hizo.

Imetolewa na
Sikika